# BRELA

**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**

ISSN:0000401 | Toleo Na. 05 | Aprili- Juni 2023




# SERA YA TAIFA YA MILIKI UBUNIFU YAJA

# YALIYOMO



SERA YA TAIFA YA MILIKI UBUNIFU YAJA 4



ALAT WATAKIWA KUJIRIDHISHA NA WAZABUNI 9



Fahamu umuhimu wa Kampuni kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa 38

## TAHARIRI

# Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu



*Bw. Godfrey Nyaisa*
*Afisa Mtendaji Mkuu BRELA*

Toleo la tano la jarida hili ni muendelezo wa majarida yanayotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Jarida hili limejikita katika kutoa elimu na taarifa za majukumu na shughuli mbalimbali zinazoendelea kutekelezwa kwa kuzingatia maboresho yanayofanyika ili kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa ufanisi na weledi. Naamini kupitia jarida hili wateja na wadau wetu watapata fursa ya kuelewa jitihada zinazofanywa na BRELA katika kuhakikisha huduma zetu zinapatikana kwa urahisi, ubora na kwa gharama nafuu. Pia, kuwa sehemu ya utatuzi wa changamoto zinazowakabili wafanyabiashara ikiwa ni pamoja na kujenga mazingira wezeshi na rafiki ya kibiashara hapa nchini.

Jarida hili limesheheni taarifa mbalimbali, makala za elimu na mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na shughuli zilizotolewa na BRELA katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2022/2023. BRELA imeendelea kuboresha utoaji wa huduma za usajili, ulinzi na kutoa elimu na mafunzo kwa makundi mbalimbali, wakiwemo wafanyabiashara, wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu na vya kati kama vile; Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino cha Tanzania (SAUT), Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Afya Bugando (CUHAS-Bugando) na Chuo cha Kiislamu cha Morogoro na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (VETA) pamoja na shule za sekondari.

BRELA imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kushiriki mikutano, warsha, makongamano na semina mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuongeza ufanisi na tija kwenye utendaji kazi. Pia, kama namna ya kuendana na wakati kwa kuzingatia ukuwaji wa kasi wa uchumi, sayansi na teknolojia duniani.

BRELA inashirikiana na wadau wake wa kimkakati wakiwa ni pamoja na wawekezaji, wafanyabiashara na wajasiriamali kwa ujumla kwenye mashauriano na vikao kazi ili kuhakikisha malengo ya BRELA yanafikiwa kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Wakala wa mwaka 2021/22 -2025/26 (Strategic Plan 2021/22 -2025/26).

BRELA imefanikiwa kukutana na wahariri wa vyombo vya habari ambao ndiyo daraja la taarifa na mawasiliano kati yetu na umma ili kuwajengea uelewa mpana wa majukumu na shughuli za BRELA pamoja na dhana mpya ya Umiliki Manufaa na utekelezaji wa Kanuni zake. Sambamba na hilo, BRELA inaendelea kuhamasisha umma umuhimu wa kurasimisha biashara na kufanya sajili mbalimbali chini ya Sheria zinazosimamiwa na Taasisi. Pia, kukumbushia wafanyabiashara wajibu wao wa kuhuisha taarifa zao, kuwasilisha mizania ya mwaka pamoja na kupata leseni za biashara na viwanda.

BRELA inaendelea na jitihada za kuhamasisha na kuelimisha umma kwa kutumia mitandao ya kijamii, kuandaa makala na vipindi maalumu vya televisheni na redio ili kuongeza uelewa miongoni mwa wananchi kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara, kusajili Alama na kulinda vumbuzi nchini.

Toleo hili lina mkusanyiko wa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya BRELA kupitia idara na vitengo, ikiwemo hafla maalum ya kuwapongeza watumishi walioonesha uhodari wao katika utendaji kazi kwa mwaka huu. Katika masuala ya usajili na ulinzi wa vumbuzi mbalimbali nchini, BRELA inabeba sura pana kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kuwa moja ya taasisi muhimu katika kuhamasisha uwekezaji nchini. Tunakutakia usomaji mwema wa jarida hili.

## BODI YA UHARIRI

**Andrew Mkapa**
**Mwenyekiti**

**Wajumbe**

Meinrad Rweyemamu
Tawi Kilumile
Abdulrahman Songoro
Neema Kitala
Tulizo Mpina
Alpha Nuhu

**Roida Andusamile**
**Katibu**

# Sera ya Taifa ya Miliki Ubunifu yaja




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji,Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah*

**Na Theresa Chilambo**

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya Sera ya Taifa ya Miliki Ubunifu (National Intellectual Property Policy)

Kauli hii imetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah aliyemwakilisha Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara katika Maadhimisho ya siku ya Miliki Ubunifu yaliyoratibiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na kufanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Dkt. Abdallah alisema kuwa kukamilika kwa Sera hii kutasaidia kutoa miongozo itakayoimarisha miundo ya kisheria na kitaasisi katika kusimamia masuala ya Miliki Ubunifu, kuwa na taratibu rahisi na wezeshi za sajili na ulinzi mbalimbali, kuimarisha ulinzi zaidi na kuongeza maeneo mapya ya ulinzi wa Miliki Ubunifu.

"Serikali chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali hususan utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blueprint), ili kuweka mazingira bora na wezeshi katika sekta zote ikiwa ni pamoja na eneo la Miliki Ubunifu ambalo linakuwa kwa kasi duniani", alisisitiza Dkt. Abdallah

**"Serikali chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali hususan utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blueprint), ili kuweka mazingira bora na wezeshi katika sekta zote ikiwa ni pamoja na eneo la Miliki Ubunifu ambalo linakuwa kwa kasi duniani", alisisitiza Dkt. Abdallah**


Aliongeza kuwa Serikali imeanza mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali za Miliki Ubunifu kwa kuwa baadhi ya Sheria hizo zimepitwa na wakati na baadhi ya maeneo hayalindwi kisheria, hivyo itakapokamilika usimamizi wa masuala ya Miliki Ubunifu utakuwa rafiki na wezeshi kwa wafanyabiashara kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya BRELA, Bi. Judith Kadege, ambaye alimuwakilisha Mwenyekiti wa Bodi hiyo, alisema kuwa mfumo wa usajili wa ulinzi wa Miliki Ubunifu Tanzania utasaidia kuweka ulinzi katika ubunifu unaofanywa na wafanyabiashara na wabunifu mbalimbali hasa katika kipindi ambacho teknolojia inaendelea kukua kwa kasi.

Awali akizungumza katika maadhimisho hayo, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa, alisema kuwa Taasisi itaendelea kuboresha mifumo yake ya ndani ya sajili na kuweka mikakati mizuri ya kuboresha huduma wanazotoa na kuvutia zaidi wabunifu wa kazi mbalimbali ili kuongeza idadi ya sajili na linzi za kazi zao pamoja na kuhakikisha wabunifu hao wanapata manufaa ya kazi hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na uanzishaji wa maadhimisho hayo, mashindano na Tuzo za Miliki Ubunifu nchini ambayo yanategemewa kuanza hivi karibuni, kushirikiana na kutembelea wadau wa Miliki Ubunifu kama vile Taasisi na Vyuo pamoja na shule ili kutoa elimu ya Hataza na masuala mengine ya Miliki Ubunifu.

Bw. Nyaisa alisema lengo ni kuhakikisha kuwa Miliki Ubunifu inatumika kama chachu ya ukuaji wa uchumi wa mtu binafsi na Taifa kwa ujumla kutokana na umuhimu wake katika maendeleo.

Kwa mwaka 2023 maadhimisho ya Miliki Ubunifu yamebeba kauli mbiu isemayo "Wanawake na Miliki Ubunifu: Kuongeza kasi ya Ubunifu katika Biashara".




*Bw. Godfrey Nyaisa*
*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA*

# Chapeni kazi kwa bidii kufikia malengo - Nyaisa

**Na Christina Njovu**

Watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wametakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa katika muda uliobaki kufikia mwisho wa mwaka 2022/2023.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, alisema hayo wakati wa hafla fupi ya kuwapongeza watumishi hodari pamoja na watumishi wote, iliyofanyika katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

"Ndugu watumishi, BRELA imefanikiwa kujijengea heshima na imani kwa Serikali na wananchi kutokana na kutoa huduma bora, kwa haraka na kwa urahisi, kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, hivyo kuwezesha kutimiza malengo yake kwa asilimia 100% au zaidi kila mwaka" alisema Bw. Nyaisa.

Aidha, Bw. Nyaisa alisisitiza kwamba ni jambo muhimu kwa BRELA kuendelea kutunza heshima na imani hiyo kwa kufanya kazi kwa bidii na kuwaelekeza wakurugenzi na wakuu wa vitengo kuhakikisha malengo yote waliojipangia yanakamilika kwa muda uliopangwa.

**"Ndugu watumishi, BRELA imefanikiwa kujijengea heshima na imani kwa Serikali na wananchi kutokana na kutoa huduma bora, kwa haraka na kwa urahisi, kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, hivyo kuwezesha kutimiza malengo yake kwa asilimia 100% au zaidi kila mwaka" alisema Bw. Nyaisa.**

Akitaja mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha mwaka 2022/2023 ambao unaelekea ukingoni, yametokana na mchango wa watumishi wote wa BRELA na kutaja baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezajii wa malengo hayo hadi kufikia Mei 9, 2023, kuwa BRELA imefanikiwa kukusanya kiasi cha TZS.Bilioni 25,237,269,777 kati ya lengo iliyojiwekea hadi kufikia mwezi Juni, 2023 la kukusanya TZS Bilioni 28,904,217,240, kiasi hicho.cha fedha ni sawa na asilimia 87 ya lengo lililowekwa kwa mwaka.

Alieleza kuwa mafanikio hayo yanatokana na BRELA kusajili Kampuni 12,398 kati ya 13,100 sawa na asilimia 95, Majina ya Biashara 23,075 kati ya 25,000 sawa na asilimia 92, Hataza 53 kati 35 sawa na asilimia 151, kutoa Hataza 16 kati ya 35, sawa na asilimia 46, maombi ya Hataza yaliyowasilishwa kupitia ARIPO ni 212 kati ya 650 sawa na asilimia 33, Alama za Biashara na Huduma 3,272 kati ya 4,120 sawa na asilimia 79, kutoa Leseni za Viwanda 160 kati ya 200 sawa na asilimia 80, kutoa vyeti vya Usajili wa Viwanda 35 kati ya 44 sawa na asimia 80, kutoa Leseni za Biashara 13,327 kati ya 13,750 sawa na asilimia 97.

# Mtwara wapongeza uboreshaji mazingira ya biashara

**Na Nehemia Mihayo**

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Mhe. Hanafi Msabaha ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa kutekeleza Mpango wa kuboresha mpango mazingira ya biashara (MKUMBI).

Mhe. Msabaha alibainisha hayo wakati akifungua mafunzo ya siku tatu ya Maafisa Biashara kutoka katika Mikoa 10 ya Tanzania Bara kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed.

Alieleza kuwa mafunzo hayo ni muhimu, hasa kwa kuzingatia kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara nchini, ili kuendana na azma ya kufanya mageuzi ya kiuchumi.

"Nawapongeza sana BRELA kwa kuandaa na kuratibu mafunzo haya muhimu kwa Maafisa Biashara, ikiwa pia ni njia mojawapo ya utekelezaji wa "Blue Print" yenye nia ya kuboresha mazingira ya biashara nchini. Juhudi hizi ni nzuri na zitaleta matokeo chanya katika ukuaji wa biashara na uwekezaji nchini", alisema Mhe. Msabaha.

Aidha alibainisha matarajio yake kuhusu mafunzo yanayotolewa kuwa yatasaidia Maafisa Biashara kubadili fikra na mitazamo na kuwa watoa huduma na msaada kwa wafanyabiashara.

Awali akizungumza na washiriki wa mafunzo hayo kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Leseni za Biashara, Bw. Tawi Kilumile alieleza kuwa lengo kuu ni kuwajengea uwezo Maafisa Biashara kusimamia Sheria ya Leseni za Biashara (Sura 208) na Sheria ya Taifa ya Usajili wa Leseni za Viwanda (Sura 46), kwa ufasaha wanapotekeleza majukumu yao na hatimaye kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

> **"Sheria hii inatafsiri yake, kuanzia kifungu cha kwanza (1) hadi cha 34. Pia imeonyesha majukumu ya kila anayehusika katika kutekeleza Sheria hii, hivyo ni vyema tukaielewa vizuri na endapo kuna eneo lenye changamoto ni vyema kuuliza ili kupata uelewa wa pamoja" alieleza Bw. Kilumile.**

Alitoa rai kwa maafisa kutokujikita katika ukusanyaji mapato kama ilivyokuwa hapo awali, bali kuwa marafiki na washauri wa wafanyabiashara kwani kukua kwa



*Baadhi ya maafisa biashara kutoka katika mikoa 10 ya Tanzania Bara wakifuatilia mafunzo juu ya Usimamizi wa Sheria ya Leseni za Biashara (Sura 208) na Sheria ya Taifa ya Usajili wa Leseni za Viwanda (Sura 46), mkoani Mtwara.*



biashara ndiyo kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali.

Katika mafunzo hayo Maafisa Biashara walipitishwa katika vifungu 34 vya Sheria ya Leseni za Biashara (Sura 208) ili kuelewa tafsiri yake na namna ya kuvisimamia wakati wa utetekelezi wa majukumu katika maeneo yao ya kazi.

Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Leseni za Biashara kutoka BRELA, Bw. Tawi Kilumile alieleza kuwa Sheria hiyo ndio mwongozo mkuu wa utekelezaji wa majukumu yao kwakuwa umetoa uelekeo kuhusu nini cha kufanyika katika kila hatua.

"Sheria hii inatafsiri yake, kuanzia kifungu cha kwanza (1) hadi cha 34. Pia imeonyesha majukumu ya kila anayehusika katika kutekeleza Sheria hii, hivyo ni vyema tukaielewa vizuri na endapo kuna eneo lenye changamoto ni vyema kuuliza ili kupata uelewa wa pamoja" alieleza Bw. Kilumile.

Alieleza kuwa tangu kupitishwa kwa Sheria hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 1972, imefanyiwa mabadiliko mara kadhaa, ili kuendana hali iliyopo hivi sasa, hivyo ni muhimu kuipitia mara kwa mara na kuielewa vizuri.

Kwa upande wake Afisa Leseni kutoka BRELA, Bw. Peter Riwa, aliwataka Maafisa Biashara kutumia mbinu mbadala za kuwahamasisha wafanyabiashara kutii sheria na kuwa na Leseni badala ya kufungia biashara zao.

Alieleza kuwa ni vyema wafanyabiashara wakaelimishwa kuhusu Sheria hii ili wafahamu kuwa kuna faini kwa mujibu wa sheria kwa kutokuwa na Leseni hivyo ni vyema kutii sheria ili kuepuka Usumbufu.

Akichangia mada katika mafunzo hayo, Afisa Leseni kutoka BRELA, Bw. Koyan Aboubakari, aliwataka Maafisa Biashara kuwasaidia wafanyabiashara kufahamu jinsi ya kupata mahitaji muhimu kwa ajili ya kupata Leseni badala ya kukataa maombi yao.

Mahitaji hayo ni pamoja na namba ya Kitambulisho cha Taifa ya mwombaji wa leseni, namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN), Uthibitisho wa sehemu ya kufanyia biashara kama mkataba wa pango, leseni ya makazi au hati.

Mahitaji mengine ni hati ya kuonyesha kutodaiwa kodi (Tax Clearance Certificate) Kibali kutoka mamlaka ya udhibiti (Kutegemea na aina ya biashara).

**"Nawapongeza sana BRELA kwa kuandaa na kuratibu mafunzo haya muhimu kwa Maafisa Biashara, ikiwa pia ni njia mojawapo ya utekelezaji wa "Blue Print" yenye nia ya kuboresha mazingira ya biashara nchini. Juhudi hizi ni nzuri na zitaleta matokeo chanya katika ukuaji wa biashara na uwekezaji nchini", alisema Mhe. Msabaha.**

Kwa kufanya hivyo watakuwa wanafanikisha lengo kuu la serikali la kukuza biashara na kutengeneza mazingira rafiki ya biashara na uwekezaji.

Maafisa Biashara walioshiriki katika mafunzo hayo ni kutoka Mikoa ya Lindi, Ruvuma, Njombe, Iringa, Songwe, Mbeya, Pwani, Morogoro Dar es Salaam na Mtwara.

# Elimu Miliki Ubunifu yawafikia wanachuo Mwanza

**Na Sheila Mfunami**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewafikiwa wahadhiri pamoja na wanafunzi zaidi ya 2,000 katika zoezi la kutoa elimu ya Miliki Ubunifu katika Vyuo Vikuu na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), jijini Mwanza.

Katika mafunzo hayo yaliyofanyika hivi karibuni Wahadhiri pamoja na Wanafunzi walielekezwa kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA, upande wa Alama za Biashara na Huduma pamoja na Hataza

Akielezea huduma zinazotolewa na BRELA kwa Wahadhiri pamoja na Wanafunzi wa Chuo VETA , Afisa Mwandamizi kutoka BRELA, Bw. Raphael Mtalima aliwataka Wahadhiri hao wanapowafundisha wanafunzi wasisite kuwakumbusha kuwa watakaporasimisha biashara zao itawafungulia wigo wa kutambulika na mamlaka mbalimbali na pia kuwawezesha kukopesheka katika Taasisi za kifedha.

BRELA inaendelea na kampeni ya kutoa elimu katika Vyuo mbalimbali nchini ili kukuza uelewa wa masuala ya Miliki Ubunifu pamoja na huduma zote zinazotolewa na Wakala.

Kampeni hii ya kutoa elimu kwa Wanafunzi vyuoni ni endelevu ambayo ilianza rasmi Mkoani Mbeya na kufuatiwa na mkoa wa Mwanza na itaendelea katika mikoa mingine nchini, lengo kuu ni kuhakikisha elimu hii inawafikia Wanafunzi wengi zaidi waliopo vyuoni.

Mafunzo ya Miliki Ubunifu Jijini Mwanza, yalifanyika katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afya na Sayansi Mwambata-Bugando, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo ( SIDO), pamoja na Chuo cha VETA.

**BRELA inaendelea na kampeni ya kutoa elimu katika Vyuo mbalimbali nchini ili kukuza uelewa wa masuala ya Miliki Ubunifu pamoja na huduma zote zinazotolewa na Wakala.**



*Baadhi ya wanafunzi wa Chuo cha Ufundi Stadi VETA cha jijini Mwanza, wakifuatilia mafunzo ya Miliki Ubunifu yaliyotolewa na BRELA chuoni hapo.*

# ALAT watakiwa kujiridhisha na wazabuni




*Bw. Godfrey Nyaisa Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA akiwasilisha mada kwenye mkutano wa ALAT uliofanyika Arusha*

**Na Nehemia Mihayo**

Wajumbe wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) wametakiwa kujiridhisha na Kampuni wanazoingia nazo mikataba ya kutoa huduma katika maeneo yao ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

Rai hiyo ilitolewa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa alipokuwa akiwasilisha mada katika mkutano wa 37 wa ALAT uliofanyika kwenye Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC), Jijini Arusha.

Bw. Nyaisa alieleza kuwa, bado kuna changamoto katika Tawala za Mikoa ya kuingia mikataba na taasisi ambazo hazitambuliki kisheria au ambazo hazijakidhi vigezo. Hali hii inasababisha upotevu mkubwa wa rasilimali za Taifa.

"Mnapotaka kuingia mikataba na Kampuni yeyote ni muhimu kujiridhisha kwa kujua kama Mzabuni huyo ni halali, kwa kuangalia kama anawasilisha mizania ya kila mwaka, wanahisa wake ni watu gani pamoja na anuani zao ili kujiridhisha", alieleza Bw. Nyaisa.

Aliongeza kuwa mara kadhaa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa halmashauri mbalimbali kuingia katika migogoro na wazabuni ambao kimsingi hawakutakiwa kuwapa zabuni kama wangepata taarifa zao kutoka BRELA.

Bw. Nyaisa alieleza kuwa, BRELA imewekeza nguvu nyingi kutoa mafunzo kwa Maafisa Biashara nchi nzima ili kuwajengea uwezo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Leseni za Biashara.

"Wakala imekamilisha awamu ya kwanza ya mafunzo kwa Maafisa Biashara wa mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa awamu ya kwanza. Utekelezaji wa awamu ya pili umeanza kwa Maafisa ambao hawakupata mafunzo katika awamu ya kwanza na mpaka sasa mikoa kumi (10) imefikiwa.

Wito wangu kwenu ni kwamba muwatumie vizuri Maafisa hao ili kuchochea urasimishaji wa biashara na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na uanzishwaji wa biashara nchini", alifafanua Bw. Nyaisa.

BRELA ilishiriki katika Mkutano huo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati wake wa elimu kwa umma.

# Gwajima aipongeza BRELA

**Na Sheila Mfunami**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Wenye Mahitaji Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb), ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa kuwa kidigitali na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Waziri Gwajima ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la BRELA katika maadhimisho ya Wiki ya Barcode Kitaifa, yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Mhe. Gwajima alisema amefurahishwa na huduma nzuri wanayopatiwa wadau wanaofika katika banda la BRELA, ambayo itaongeza idadi kubwa ya wafanyabiashara waliorasimisha biashara.

"Nimefurahishwa sana na huduma nzuri inayotolewa na BRELA, hivyo basi wafanyabiashara ambao bado hawajarasimisha biashara zao ni vyema wakafuata taratibu sahihi za sajili," alisisitiza Mhe. Gwajima.

Aidha Mhe. Waziri alitoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa na kurasimisha Biashara zao.

Katika maadhimisho hayo yaliyokwenda sambamba na maonesho ya wajasiriamali, BRELA ilitumia fursa hiyo kuwahamasisha wadau kurasimisha biashara zao huku ikiendelea kutoa usaidizi katika mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao pamoja na kutoa huduma za papo kwa papo.

**"Nimefurahishwa sana na huduma nzuri inayotolewa na BRELA, hivyo basi wafanyabiashara ambao bado hawajarasimisha biashara zao ni vyema wakafuata taratibu sahihi za sajili," alisisitiza Mhe. Gwajima.**




*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na wenye Mahitaji Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano Bi. Roida Andusamile, juu ya huduma zinazotolewa na BRELA alipotembelea banda la BRELA kwenye maadhimisho ya Wiki ya Barcode Kitaifa Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*

# BRELA yawatambua Wabunifu

**Na Theresa Chilambo**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetoa tuzo kwa Wabunifu sita wa Kitanzania ikiwa njia mojawapo ya kutambua mchango wao katika ukuaji wa sekta ya biashara na afya nchini.

Tuzo hizo zilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, katika maadhimisho ya Siku ya Miliki Bunifu Duniani iliyofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Tuzo ya kwanza ilienda kwa Eliot Company Ltd. mfanyabiashara mwenye Alama ya Biashara ya “Active Mama” ambapo bidhaa yake ilisajiliwa mwaka 2018 na bidhaa yake imekaa sokoni kwa miaka saba sasa na imesambaa katika mikoa 26. Hadi sasa amefanikiwa kutoa ajira kwa watu 25.

Tuzo ya pili ilienda kwa mmiliki wa kampuni ya Natureripe Kilimanjaro Ltd. Mfanyabiashara mwenye alama ya biashara ya Naturepipe iliyosajiliwa mwaka 2006 na imekaa sokoni kwa miaka 23. Bidhaa hizo kwa sasa zinapatikana ndani na nje ya nchi ya Tanzania kama vile Dubai, Qatar, Australia, Uingereza na ameweza kutoa ajira kwa watu 43. Kampuni hiyo pia imefanikiwa kutunza mazingira kwa kupanda miti na kutumia mabaki yanayotokana

**Mawanda ya umiliki umejikita katika kulinda alama za biashara na taarifa za TEHAMA. Bunifu zao zimejikita katika kutoa huduma kwa watu wa kipato cha chini na wamefanikiwa kuwafikia watu mbalimbali wakiwa na malengo ya kufikia watu milioni mbili.**




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah akimkabidhi tuzo mwakilishi wa Kampuni ya LAMATA Village Entertainment aliyewainua na kuwawezesha watu wengine kupitia Hakimiliki kwa kuongeza ajira.*

na malighafi zilizotumika kwa ajili ya kuboresha mazingira kwa maendeleo endelevu.

Tuzo ya tatu ilitolewa kwa Bw. Emmanuel Mushi akiwa ni Mbunifu aliyetumia Miliki Ubunifu (Hataza) kwa ajili ya kusaidia jamii. Bw. Mushi alivumbua Automatic Modified Neonatal Incubator iliyosajiliwa mwaka 2020. Vumbuzi yake imesaidia kuwakuza watoto njiti 2,000.

Uzinduzi wa kifaa chake ulifanyika na Taasisi ya Costech 2019. Hataza yake hadi sasa inatumika katika mkoa wa Manyara.

Tuzo ya nne ilitolewa kwa kampuni ya LAMATA Village Entertainment inayoongozwa na Bi. Leah Mwendamseke maarufu kwa jina la LAMATA. Tuzo yake imetambulika kama mbunifu aliyewawezesha wengine kupitia Miliki Ubunifu kwa kutoa ajira kwa watu 100 na kukuza kipato kupitia filamu ya Jua Kali.

Tuzo ya tano ilitolewa kwa Fahamu Sheria Foundation kwa ubunifu wa kuwa na mfumo wa Sheria Kiganjani. Alisajili alama ya biashara mwaka 2021 na amefanikiwa kutumia aina mbili za Miliki Ubunifu ambazo ni Alama za Biashara na Hatimiliki. Mawanda ya umiliki umejikita katika kulinda alama za biashara na taarifa za TEHAMA. Bunifu zao zimejikita katika kutoa huduma kwa watu wa kipato cha chini na wamefanikiwa kuwafikia watu mbalimbali wakiwa na malengo ya kufikia watu milioni mbili.

Tuzo ya Sita ilitolewa kwa mmiliki wa kampuni ta NN General Supplies yenye alama ya biashara ya HQ . Kupitia bidhaa zake, imesaidia jamii kwa kusambaza taulo za kike kwa bei nafuu.

Dkt. Abdallah aliwapongeza wabunifu waliopata tuzo na na kusisitiza kuwa tuzo hizo ziwe chachu ya kukuza ubunifu katika biashara ili wengine waone umuhimu wa kuendeleza na kukuza ubunifu katika shughuli za kibiashara na maisha ya kila siku.

BRELA itaendelea kuhamasisha wafanyabiashara kusajili Alama za Biashara na Huduma na wavumbuzi kupata Hataza ili kazi zao ziweze kulindwa kisheria.

# “Lindeni Bunifu zenu ziwanufaishe”



*Wanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe wakifuatilia mafunzo yaliyotolewa na BRELA chuoni hapo*

**Na Njwaba Mwijibe**

Baadhi ya wahadhiri na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), wamekumbushwa kulinda Bunifu zao Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ili ziwanufaishe.

Kauli hiyo ilitolewa na Afisa Sheria kutoka BRELA Bw. Abdulkarim Nzori wakati wa mafunzo yaliyofanyika chuoni hapo hivi karibuni, yaliyolenga kuwajengea uwezo Wahadhiri pamoja na Wanafunzi kuhusu masuala ya Miliki Ubunifu.

Alisema kuwa Chuo cha Sayansi na Teknolojia kinakuwa na tafiti mbalimbali ambazo matokeo yake kwa namna moja yanaweza kufanyiwa mchakato wa kuwa bidhaa au namna za kutengeneza vitu mbalimbali hivyo, wakilinda vumbuzi hizo ztakuwa na manufaa kwao binafsi na kwa jamii pia.

Aliongeza kwa mifano kuwa haki za Miliki Ubunifu ikiwemo Hataza na Alama za Biashara na Huduma zimekuwa na thamani ulimwenguni hivyo Bunifu wanazo zianzisha au zibuni wazisajili BRELA ili viwanufaishe na zisaidie jamii.

Awali akitoa neno la Ufunguzi Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Elimu, Tafiti na Ushauri, Prof. Godliving Mtui aliwapongeza BRELA kwa kuandaa mafunzo hayo ya Miliki Ubunifu na kufika katika Chuo hicho ambacho moja kwa moja kinajihusisha katika masuala ya Sayansi na Teknolojia.

Pia aliwataka BRELA kuendelea kufika katika chuo hicho pale wanapopewa mialiko na kutoa mafunzo kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA.

Wakitoa mafunzo katika Chuo Kikuu Mzumbe Jijini Mbeya, Afisa Sheria kutoka BRELA Bw. Abdulkarim Nzori alisema Bunifu mbalimbali zikitumiwa zinaweza kutatua changamoto katika jamii na kuwakuza kiuchumi wabunifu na wafanyabiashara.



Katika mafunzo hayo yaliyohudhuriwa na wanafunzi zaidi ya 1000, walielekezwa namna wanavyoweza tumia bunifu zao kujikwamua kiuchumi na kutengeneza ajira kwa watu wengine.

Wanafunzi hao pia walipata fursa ya kukumbushwa kuwa Miliki Ubunifu ni mali inayotokana na mtu kutumia akili kubuni vitu mbalimbali hivyo wabunifu na wafanyabiashara wanayo nafasi kutumia bunifu zao kama vile Alama za Biashara na Huduma zilizosajiliwa BRELA kutambulisha bidhaa au huduma wanazitoa na wanaweza kuziuza au kuzikodisha Alama hizo pale inapobidi hivyo kunufaika na bunifu zao.




*Afisa Sheria wa BRELA Bw. Abdulkarim Nzori*

Awali akitoa neno la utangulizi Afisa Sheria kutoka BRELA Bi. Grace Umoti aliwahamasisha wanafunzi hao kuchangamkia fursa ya ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Miliki Ubunifu inayotolewa na BRELA pindi nafasi hizo zinapotangazwa ili kujiongezea ujuzi na kupanua wigo wa watalamu katika nyanja ya Miliki Ubunifu

Maafisa wa BRELA walitoa pia Mafunzo katika Vyuo Vikuu na vyuo vya Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) katika Jiji la Mbeya.






*Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah alimkabidhi Tuzo mvumbuzi Emmanuel Mushi, aliyetumia Miliki Ubunifu (Hataza) kusaidia jamii. Hataza hiyo inayojulikana kama AUTOMATIC MODIFIED NEONATAL INCUBATOR, imesaidia kuwakuza zaidi ya watoto 2,000 waliozaliwa njiti katika mkoa wa Manyara. Hafla hiyo imefanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.*



*Afisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Calvin Rwambogo akifafanua jambo kwa mwanachuo wakati wa maonesho ya ubunifu yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah(katikati) akikabidhi tuzo kwa Mbunifu wa Mfumo wa Sheria Kiganjani, Fahamu Sheria Foundation ambaye amesajili alama ya biashara mwaka 2021 na kufanikiwa kutumia aina mbili za Miliki Ubunifu ambazo ni Alama za Biashara na Haki Miliki, Mawanda ya umiliki umejikita katika kulinda alama za biashara na taarifa za TEHEMA. Bunifu zao zimejikita zaidi Katika kuto a huduma za watu wa kipato cha chini. Hafla hiyo ilifanyika hivi karibuni katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.*




*Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Hataza kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bi. Neema Kitala(kushoto) akifafanua jambo kwa Mfanyabiashara Bi. Naomi Mwasambili katika eneo lake la Biashara Forest Mpya, Jijini Mbeya walipomtembelea hivi karibuni na kumshauri kusajili Alama zake za Biashara anazozitumia katika bidhaa zinazotengezwa kupitia zao la kakao ili atambulishe bidhaa hizo sokoni na kuepuka hatari ya kuibiwa Alama hizo na watu wengine. Mfanyabiashara huyo mwenye Kampuni ya Livy Africa Limited amefurahishwa na ujio wa BRELA na tayari ameanza utaratibu wa kusajili Alama za Biashara ambazo tayari zinafanya vizuri sokoni.*



*Kaimu Mkuu wa sehemu ya Hataza wa BRELA, Bi. Neema Kitala akiwahamasisha Wakufunzi na Wanafunzi wa Chuo kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), pamoja na wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari zilizo jirani na chuo hicho wapatao 700, kuchangamkia fursa za kurasimisha biashara zao BRELA pamoja na manufaa yanayotokana na urasimishaji.*




*Afisa kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Calvin Rwambogo ( kushoto) na aliyekuwa Afisa wa BRELA Bw. Raphael Mtalima (katikati kushoto) wakitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA hasa Hataza kwa wadau mbalimbali waliotembelea maonesho ya wiki ya Utafiti na Uvumbuzi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hivi karibuni. Maonesho hayo yalilenga kuchochea vumbuzi mbalimbali kwa lengo la kukuza uchumi wa Tanzania.*



***Afisa Leseni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Fransice Filimbi, akitoa mada kuhusu umuhimu wa kupata Leseni za Viwanda, Kusajili Viwanda Vidogo pamoja na huduma za Sajili nyingine zinazotolewa na BRELA katika mkutano wa wachimbaji Wadogo wa Madini na Wadau wa Madini ya Viwandani. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es Salaam.***



***Mwanamuziki na Mfanyabiashara Bi. Zuwena Yusuph maarufu kwa jina la "Shilole" amehuisha taarifa za Jina la Biashara yake Shishi Food katika Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS), hivi karibuni Kijitonyama Mabatini, jijini Dar es Salaam. Baada ya kukamilisha mchakato huo, Shilole aliwataka wafanyabiashara wengine wanaotumia majina ya biashara bila ya kuyasajili BRELA, kuyasajili ili kuyalinda kisheria na kuepuka watu wengine kujinufaisha nayo. Pia ameipongeza BRELA kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuwafikia wadau popote walipo na kuwapatia huduma.***




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa (kushoto) akimkabidhi cheti mtumishi hodari wa Taasisi, Bw. Seka Kasera, wakati wa hafla ya kuwapongeza watumishi kwa utendaji kazi bora ulioiwezesha Taasisi kufikia malengo, Hafla hiyo ilifanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam.*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa (aliyeketi katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Idara pamoja na Watumishi hodari waliochaguliwa kutoka idara mbalimbali za Taasisi katika hafla ya kuwapongeza watumishi hao kwa utendaji kazi bora ulioiwezesha Taasisi kufikia malengo. Hafla hiyo ilifanyika hivi karibu jijini Dar es Salaam.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, akimkabidhi cheti cha Udhamini Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa, kwa kutambua mchango wa Taasisi katika kuwezesha kufanyika kwa Mkutano wa 37 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania hivi karibuni, katika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC), Jijini Arusha.*



*Wakuu wa Taasisi zinazohusika na masuala ya Miliki Ubunifu Kanda ya Afrika, wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mkutano huo uliofanyika Kigali, Rwanda. Tanzania ikiwa ni mwanachama wa Shirika la Miliki Ubunifu Kanda ya Afrika (ARIPO), iliwakilishwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa. Mkutano huo uliratibiwa na ARIPO kwa kushirikiana na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani(WIPO).*



*Maafisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wakiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Rasi( Principal) wa Chuo Mzumbe, Ndaki ya Mbeya, Dkt. Kennedy Makafu (wa pili kutoka kulia), mara baada ya kufanya mazungumzo ofisini kwake walipotembelea chuo hicho hivi karibuni kwa ajili ya mafunzo ya Miliki Ubunifu. Kutoka kushoto ni Bw. Abdulkarim Nzori, Bi. Neema Kitala na kulia ni Bi. Grace Umoti.*



*BRELA wakijiandaa na maandamano ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi 2023).*



***Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania Mhe. Wiebe De Boer (katikati) na ujumbe wake wakiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya BRELA, walipotembelea ofisi za Taasisi hiyo jijini Dar es Salaam.***



***Makamu Mkuu wa Chuo cha Mtakatifu Augustino (SAUT) cha Jijini Mwanza, Prof. Costa Mahalu (kulia) akizungumza na Maafisa wa BRELA walipomtembelea ofisini kwake kabla ya mafunzo ya Miliki Ubunifu kwa Wahadhiri na Wanafunzi wa chuo hicho hivi karibuni.***

# BRELA yawapiga msasa wahadhiri Bugando

**Na Sheila Mfunami**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni BRELA imetoa mafunzo katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afya na Sayansi Mwambata cha Bugando jijini Mwanza, ili kuongeza uelewa kuhusu Miliki Ubunifu.

Akizungumza katika Mafunzo hayo hivi karibuni Chuoni hapo, Afisa Mwandamizi kutoka BRELA Bw. Raphael Mtalima alisema Bunifu mbalimbali zikitumiwa zinaweza kutatua changamoto ikiwemo za Afya katika jamii na kuwakuza kiuchumi wabunifu na wafanyabiashara.

Katika mafunzo hayo yaliyohudhuriwa na wahadhiri na watumishi wa kada mbalimbali wa Chuo hicho walielekezwa namna wanavyoweza tumia bunifu zao kutatua changamoto za Afya na Sayansi ya Tiba ili kujikwamua kiuchumi na kutengeneza ajira kwa watu wengine.

Wakufunzi hao pia walipata fursa ya kukumbushwa kuwa Miliki Ubunifu ni mali kama mali nyingine japo haishikiki na wala haionekani, inayotokana na mtu kutumia akili kubuni vitu mbalimbali, hivyo wabunifu na wafanyabiashara wanayo nafasi kutumia bunifu zao kama vile Hataza, Alama za Biashara na Huduma zilizosajiliwa BRELA kutambulisha bidhaa au huduma wanazitoa na kuziuza au kuzikodisha alama hizo pale inapobidi hivyo kunufaika na bunifu zao.

Maafisa wa BRELA pia walitoa Mafunzo katika Vyuo Vikuu mbalimbali vilivyopo jijini Mwanza, ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Tanzania cha Mtakatifu Agustino (SAUT), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) pamoja na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (VETA) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).



*Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Bugando wakifuatilia Mafunzo ya Miliki Ubunifu*




*Afisa Usajili wa BRELA, Bw. Stanislaus Kigosi (kulia) akitoa maelezo kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Thobias Andengenye (wa kwanza kushoto) alipotembelea banda la Taasisi hiyo wakati wa maonesho ya 6 ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yaliyofanyika Mkoani Kigoma.*

# RC Kigoma aridhishwa na utendaji wa BRELA

**Na Christina Njovu**

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Thobias Andengenye ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa jitihada inazozifanya za kuwezesha wananchi kurasimisha biashara zao na namna ilivyotoa huduma katika Maonesho ya sita (6) ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Pongezi hizo alizitoa alipotembelea banda la BRELA kabla ya kufunga maonesho hayo ambayo yalifanyika hivi karibuni katika uwanja wa Mwanga, Mjini Kigoma.

Mhe. Andengenye alisema ameridhishwa na namna BRELA inavyotekeleza majukumu yake, wakati akipatiwa maelezo na Afisa Usajili wa BRELA Bw. Stanislaus Kigosi, juu ya ushiriki wa BRELA katika maonesho hayo.

Akitoa maelezo hayo kwa Mkuu wa Mkoa, Bw. Kigosi, alieleza kuwa katika maonesho hayo mbali na kutoa elimu pia wamekua wakitoa usaidizi kwa wadau mbalimbali kwenye Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao, pamoja na kutoa huduma za usajii za papo kwa papo.

"Huduma zote za BRELA zinazotolewa kwa njia ya mtandao, hivyo baadhi ya wananchi wamekuwa wakipata changamoto katika kupata huduma hizo, uwepo wetu hapa ni kuwawezesha kupata huduma hizo zikiwemo Usajili wa Majina ya Biashara, Usajili wa Makampuni na Utoaji wa Leseni za Biashara Kundi "A" papo kwa papo", alisema Bw. Kigosi.

Aidha, Bw. Kigosi alizitaja huduma zingine zinazotolewa na BRELA kuwa ni pamoja na Usajili wa Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Hataza, Utoaji wa Leseni za Viwanda na huduma baada ya usajili.

Katika maonesho hayo pia maafisa wa BRELA walipata fursa ya kutembelea mabanda ya washiriki wengine na kuwahamasisha kurasimisha biashara zao.

# Peramiho wahimizwa kurasimisha biashara

**Na Njwaba Mwaijibe**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) na Mbunge wa Jimbo la Perahimo, Mhe. Jenista Mhagama, amewataka wananchi wa Jimbo hilo kurasimisha biashara zao ili kwenda na wakati na kujiletea maendeleo ya uhakika.

**"Hili ni kwenu wananchi elimu hii ambayo ni muhimu muifanyie kazi na hakika mtaona manufaa yake kwani sisi ni wazalishaji wazuri wa mahindi na tunafanya biashara, hivyo tukisajili itakuwa rahisi hata kufanya biashara na mataifa mengine", aliongeza Waziri Mhagama.**

Waziri Mhagama aliyasema hayo wakati wa kuhitimisha mafunzo ya siku moja kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho mkoani Ruvuma, yaliyotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Mhe. Mhagama alisema kuwa wananchi wa Songea kwa ujumla wamekuwa wakijishughulisha na kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi, hivyo kutokurasimisha biashara zao BRELA kunasababisha kukosa manufaa mengi zaidi.

Mhe. Mhagama alitumia fursa hiyo pia kuipongeza BRELA kwa kufanikisha mafunzo kuhusu huduma inazozitoa kwani wamekuwa lango la kufungua biashara nchini, hivyo wananchi wa Peramiho watanufaika na elimu hiyo.

"Niwapongeze BRELA mmefanya jambo zuri sana kufika katika eneo hili na kukutana na wananchi hawa na inaonesha wameelewa na watafanyia kazi, hivyo BRELA tutawahitaji wakati mwingine mje msajili hapa hapa watu wapate vyeti vyao, naomba salamu hizi mzifikishe kwa Afisa Mtendaji Mkuu na tunashukuru sana sisi wana Peramiho", aliongeza Waziri Mhe. Mhagama.

Wakati huo huo Waziri Mhagama aliwakumbusha wananchi kuchangamkia fursa ya mafunzo hayo kwa kuanza mchakato wa kujisajili BRELA ili kupata manufaa zaidi.

"Hili ni kwenu wananchi elimu hii ambayo ni muhimu muifanyie kazi na hakika mtaona manufaa yake kwani sisi ni wazalishaji wazuri wa mahindi na tunafanya biashara, hivyo tukisajili itakuwa rahisi hata kufanya biashara na mataifa mengine", aliongeza Waziri Mhagama.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliwakutanisha wananchi zaidi ya 600 kutoka katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambayo yameratibiwa na BRELA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mbunge wa Peramiho.




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu na (Mb), Mhe. Jenista Mhagama akifungua mafunzo ya siku moja kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho yaliyotolewa na BRELA*

# DIT wajengewa uwezo kuhusu Miliki Ubunifu



*Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Miliki Ubunifu BRELA, Bi. Loy Mhando akitoa ufafanuzi juu ya huduma za Hataza kwa wahadhiri wa Chuo cha Teknolojia Cha Dar es Salaam (DIT), walipotembelea ofisi za BRELA jijini Dar es salaam.*

**Na Lugano Mwakyombe**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa elimu kwa wahadhiri wa Chuo cha Teknolojia Cha Dar es Salaam (DIT), kwa lengo la kuwajengea uwezo kuhusu Milki Ubunifu (IP). Elimu hiyo ilitolewa hivi karibuni kwa wahadhiri hao waliofika katika ofisi za BRELA na kujifunza jinsi ya uchakataji wa maombi ya Alama za Biashara na huduma pamoja na Hataza.

Akizungumza kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu, Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu Bi. Loy Mhando alibainisha kuwa amefurahishwa ujio huo kwa kuwa unaonesha dhamira ya dhati ya kuhitaji kujua/kufahamu zaidi kuhusu huduma zinazotolewa na Taasisi hiyo.

"Mara nyingi Taasisi imekuwa ikifanya jitihada kuwafuata wadau wake katika maeneo yao ili kuwapa elimu. Kitendo hiki cha kufika katika ofisi ya BRELA ni dhamira ya dhati na kiu ya kujifunza kuhusu huduma zinazotolewa hapa. Ni imani yangu kwamba elimu mtakayoipata hapa itawasaidia siku zote" alisema Bi Mhando.

Naye Mkuu wa Sehemu ya Alama za Biashara na Huduma wa BRELA, Bw. Seka Kasera alieleza kuwa mbali na Usajili wa Alama za Biashara na Huduma na Hataza, taasisi pia inatoa huduma nyingine nne. Alizitaja huduma hizo kuwa ni pamoja na Usajili wa Kampuni, Majina ya Biashara, Leseni za Biashara kundi "A" na Leseni za Viwanda na kusisitiza kuwa huduma zote kwa sasa zinatolewa kwa njia ya mtandao.

**"Mara nyingi Taasisi imekuwa ikifanya jitihada kuwafuata wadau wake katika maeneo yao ili kuwapa elimu. Kitendo hiki cha kufika katika ofisi ya BRELA ni dhamira ya dhati na kiu ya kujifunza kuhusu huduma zinazotolewa hapa. Ni imani yangu kwamba elimu mtakayoipata hapa itawasaidia siku zote" alisema Bi Mhando.**

Wahadhiri hao walifanya ziara hiyo ya mafunzo kwa ili kuongeza maarifa yatakayowawezesha kuwafundisha wabunifu waliopo katika chuo hicho ili wanapozalisha bunifu mbalimbali wazilinde kisheria.

# BRELA yakutana na Vyombo vya Uchunguzi



*Washiriki kutoka vyombo vya uchunguzi wakihudhuria mafunzo ya Kanuni za Wamiliki Manufaa yaliyotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), jijini Mbeya.*

**Na Peter Tweve**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imevitaka vyombo vya uchuguzi nchini kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Kanuni za Wamiliki Manufaa, ili wamiiki wa Kampuni wafanye shughuli zao kwa uwazi na uadilifu.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Sehemu ya Usajili wa Kampuni wa BRELA, Bw. Isdory Nkindi wakati wa warsha ya kuhamasisha utekelezaji wa Kanuni za Wamiliki Manufaa, iliyowashirikisha maafisa kutoka vyombo vya uchunguzi, Jijini Mbeya.

Bw. Nkindi alitumia fursa hiyo kuwambusha wamiliki wa Kampuni kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa BRELA, ili ziweze kufanyiwa kazi.

"Taarifa za Wamiliki Manufaa zinalisaidia Taifa katika mambo mbalimbali ikiwemo kijiepusha na masuala ya ugaidi na utakatishaji fedha, hivyo ninyi kama vyombo vya uchuguzi ni muhimu kuwahimiza wamiliki wa Kampuni kuwasilisha taarifa hizi kama kanuni za Wamiliki Manufaa zinavyotaka", amesema Bw. Nkindi.

Kwa upande wake Msajili Msaidizi wa BRELA, Bi. Leticia Zavu aliwashukuru maafisa wa vyombo vya uchunguzi kwa kuendelea kushirikiana na BRELA kwani kanuni hizo zikitekelezwa kikamiifu kunakuwa uwazi katika utendaji kazi.

Warsha hiyo ya siku moja ililenga kuongeza uelewa juu ya masuala ya Wamiliki Manufaa.

**"Taarifa za Wamiliki Manufaa zinalisaidia Taifa katika mambo mbalimbali ikiwemo kijiepusha na masuala ya ugaidi na utakatishaji fedha, hivyo ninyi kama vyombo vya uchuguzi ni muhimu kuwahimiza wamiliki wa Kampuni kuwasilisha taarifa hizi kama kanuni za Wamiliki Manufaa zinavyotaka", amesema Bw. Nkindi.**

# Temeke waridhishwa na utendaji kazi wa BRELA

**Na Lugano Mwakyombe**




*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Bw. Elihuruma Mabelya akisalimiana na Afisa Usajili Mwandamizi wa BRELA Bw. Nassoro Mtavu alipotembelea banda la Wakala hiyo katika Tamasha la Kijana Janjaruka na Fursa.*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imepogezwa kutokana na jitihada inazozifanya za kutoa elimu na mafunzo kwa jamii ili kukuza uelewa wa wananchi inaowahudumia.

Pongezi hizo zilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Temeke Bw. Elihuruma Mabelya, alipotembelea banda la BRELA katika "Tamasha la kijana Janjaruka na Fursa". Ililolofanyika hivi karibuni katika viwanja vya Zakhiem- Mbagala, Jijini Dar es Salaam.

Akiwa katika banda la BRELA Mkurugenzi huyo alishuhudia muitikio wa wananchi wa Temeke katika kupata elimu na huduma za papo kwa papo zinazotolewa na Taasisi katika tamasha hilo.

Awali Mkurugenzi huyo alielezwa na Afisa Usajili Mwandamizi wa BRELA Bw. Nassoro Mtavu namna BRELA inavyoshiriki kutoa elimu kwa umma mbali ya kushiriki kwenye matamasha na maonesho mbalimbali, kuwa ni pamoja na kutembelea Taasisi za elimu ya juu na ya kati, kushiriki katika semina na makongamano pamoja na kutoa elimu kwa njia ya redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Bw. Mtavu aliwasihi wananchi wa Temeke kutumia fursa iliyopo kwa kufika katika banda la BRELA ili kupata huduma na kutatuliwa changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wakati wa usajili katika mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao.

Wakati huo huo Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Wilaya ya Temeke, Mhe. Abdallah S. Mtinika alipotembelea banda la BRELA ameiomba kuendelea kusaidia vijana wa Wilaya ya Temeke ili waweze kurasimisha biashara zao.

"BRELA muandae programu mbalimbali za kuwashirikisha vijana wa Temeke ili waweze kutoka kwenye utegemezi na kufikia hatua ya kujisimamia kwa

> **"BRELA muandae programu mbalimbali za kuwashirikisha vijana wa Temeke ili waweze kutoka kwenye utegemezi na kufikia hatua ya kujisimamia kwa kuwa fursa zipo nyingi" alisisitiza Mhe. Mtinika**

kuwa fursa zipo nyingi" alisisitiza Mhe. Mtinika

Naye Nassoro Mtavu, Msaidizi wa Usajili Mwandamizi kutoka BRELA, alieleza kuwa BRELA inatoa mafunzo kuanzia ngazi za vyuoni na pia wale walio nje ya mfumo wa elimu, huwafikia kwa kushiriki kwenye matukio mbalimbali yanayoratibiwa kuanzia ngazi za wilaya.

"Kwa upande wa vyuoni vijana wamekuwa na bunifu zao bila ya kujua namna ambavyo wanaweza kuzilinda bunifu hizo na kuzitumia kibiashara" amesema Bw. Mtavu

Bw. Mtavu alisisitiza kuwa BRELA imeweza kutambua mchango wa vijana hao hasa kupitia maadhimisho ya siku ya Miliki Ubunifu Duniani ambapo Tanzania iliadhimisha tarehe 28 Aprili,2023 kupitia alama zao walizosajili, BRELA ilitambua ubunifu wao na kuwatunukia tuzo ikiwa ni sehemu ya kuthamini mchango wao katika ukuaji wa sekta ya biashara nchini, kutoa ajira na kuwepo kwa alama ya biashara ambayo bidhaa yake imedumu kwenye soko la biashara kwa muda mrefu

BRELA ilishiriki kwenye Maonesho ya Kijana Janjaruka Festival Temeke ya Fursa kwa kutoa huduma mbalimbali za Sajili, utoaji wa Leseni na huduma baada ya Sajili.

# Wahariri watakiwa kuwa mabalozi wa BRELA




*Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania Bw. Deodatus Balile*

**Na Nehemia Mihayo**

Wahariri wa Vyombo vya habari nchini, wametakiwa kuwa mabalozi wazuri kwa Wananchi kuhusu dhana ya Umiliki Manufaa katika Kampuni kwa kuwapa taarifa sahihi kupitia vyombo vya habari ambavyo wanavitegemea.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania, Bw. Deodatus Balile katika Warsha ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na wahariri hao iliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC).

Bw. Balile ambaye alikuwa Mgeni Rasmi katika Warsha hiyo alieleza kuwa zoezi hilo linafanyika mahususi kwa ajili ya kupeana uzoefu na uelewa wa pamoja ili kuifikishia jamii taarifa sahihi.

"Baada ya Warsha hii, ni imani yangu kwamba mtakuwa mmepata uelewa wa kutosha ambao utawasaidia kuwakumbusha Watanzania juu ya muda, taratibu na umuhimu wa uwasilishaji wa taarifa




*Mkurugenzi wa Leseni Bw. Andrew Mkapa*



***Baadhi ya wahariri wa vyombo vya habari wakifuatilia mafunzo***

za Wamiliki Manufaa katika Kampuni kwa mujibu wa sheria", alisema Bw. Balile.

Awali akitoa hotuba ya ukaribisho kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Mkurugenzi wa Leseni, Bw. Andrew Mkapa alieleza kuwa Wakala inatambua kuwa wahariri ni kiungo muhimu katika kuhamasisha urasimishaji biashara nchini.

"BRELA inatambua mchango wa Wahariri kwenye utekelezaji wa shughuli zake na kwa sababu hiyo imekuwa ikiwashirikisha kuhusu marekebisho na maboresho mbalimbali yanayofanyika au yanayoendelea kisheria na kimfumo lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi wakati wote", alisema Bw. Mkapa.

Uwasilishaji wa taarifa za Miliki Manufaa unatokana na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitisha marekebisho ya Sheria ya Kampuni, Sura 212 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Kampuni zilizosajiliwa na zinazoendelea kusajiliwa.

Mwaka 2022, Kanuni za Umiliki Manufaa katika Kampuni zilipitishwa na kuanza kutumika rasmi, malengo makuu yakiwa ni kuboresha mazingira rafiki ya uwekezaji, kuzuia ukwepaji kodi pamoja na kudhibiti utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya kigaidi.



***Baadhi ya wahariri wa vyombo vya habari wakifuatilia mafunzo***

# BRELA ilivyoshiriki Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani

**Na Waandishi Wetu**

Maafisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wameshiriki katika maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) mkoani Morogoro na jijini Dar es Salaam ambapo kitaifa yamefanyika katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiye aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya kitaifa. Jijini Dar es salaam maadhimisho yamefanyika kimkoa katika Uwanja wa Uhuru uliopo Wilaya ya Temeke.

Kauli mbiu kwa mwaka huu ni "Mishahara Bora na Ajira za Staha ni nguzo kwa maendeleo ya Wafanyakazi" Wakati ni Sasa!

Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe. Mwanahamisi Munkunda, ndiye aliyekuwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho hayo jijini Dar es Salaam.




*Watumishi wa BRELA wakiandamana katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, ngazi ya mkoa, yaliyofanyika Temeke Jijini Dar es Salaam.*



*Watumishi wa BRELA wakifuatilia maandamano ya Taasisi mbalimbali za serikali na binafsi wakati wa kuingia Uwanjani kwenye Maadhimisho Siku ya Wafanyakazi Duniani, ngazi ya mkoa yaliyofanyika Temeke Jijini Dar es Salaam.*



*Watumishi wa BRELA wakisikiliza hotuba ya Mgeni rasmi katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ngazi ya mkoa yaliyofanyika Temeke Jijini Dar es Salaam.*




*Watumishi wa BRELA wakiandamana katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, yaliyofanyika Kitaifa jijini Morogoro*



# Wanafunzi Chuo Kikuu cha Kiislamu wapewa elimu ya biashara



*Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM), wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya maafisa wa BRELA walipotembelea ofisi za Taasisi hiyo.*

Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro(MUM), wametakiwa kukabiliana na changamoto za ajira, mara baada ya kuhitimu masomo yao kwa kufanya biashara na kuzirasimisha Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni ( BRELA).

Rai hiyo imetolewa na Afisa Usajili wa BRELA Bw. Lumambo Shiwala wakati akiwasilisha mada kuhusu usajili wa majina ya biashara na Makampuni kwa wanafunzi wa chuo hicho, waliofanya ziara ya mafunzo katika ofisi za BRELA tarehe 17 Mei, 2023, jijini Dar es Salaam.

Wanafunzi hao wa mwaka wa Pili ngazi ya Diploma ya Sheria na Usimamizi wa Biashara wamehamasishwa kwa kuhakikisha kuwa baada ya kuhitimu masomo yao wakabiliane na changamoto ya ukosefu wa ajira kwa kuanzisha biashara na kuzirasimisha BRELA ambazo zitawawezesha kupata fursa za mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha.

Aidha, Bw. Shiwala amesema kuwa Usajili wa Majina ya Biashara, Makampuni, Alama za Biashara na Huduma, pamoja na Utoaji wa Leseni za Biashara Kundi "A" na Leseni za Viwanda zote zinazosimamiwa na kulindwa na BRELA, zinafanyika kwa njia ya mtandao, lengo likiwa ni kuokoa muda na kupunguza gharama.

Kwa upande wake Mhadhiri kutoka Chuo hicho Bw. Habibu Siraji, ameishukuru BRELA kwa elimu waliyoipata na kuahidi kuwa mabalozi wazuri wa BRELA.



*Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM), wakifuatilia mafunzo yaliyokuwa yakitolewa na wataalamu wa BRELA.*

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# A CALL FOR COMPANIES TO FILE ANNUAL RETURNS

The Registrar of Companies calls all companies incorporated and registered in Tanzania to file their annual returns/financial statements as required by the Companies Act, CAP 212.

**HOW TO FILE ANNUAL RETURNS & FINANCIAL STATEMENTS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM**

1. Log in on the Online Registration System (ORS).
2. Select 'e - service'.
3. Select 'Company' .
4. Select 'Filing of annual return (accounts) / Update.'
5. Fill in Incorporation/Compliance number.
6. Fill in company's details.
7. Upload form 128 together with a signed and dated consolidated form.
8. Select mode of payment (Mobile or Bank).
9. After payment the application will be received for review.

**Note:** Filing fee of an annual return is Tzs. 22,000 / - if submitted on time. Delayed submission of an annual return attracts a late filing fee of Tzs. 2500 / - (compounded) per every delayed month or part thereof.

**BRELA HOUSE**
Plot No 23, Block No. 20,
Sokoine Drive/Shaaban Robert Street,
P.O Box. 9393, 11101
Ilala, Dar es Salaam.

**DODOMA OFFICE**
PSSF Building
Makole Street 10th Floor

*"We give legal life to your business"*

Telephone:+ 255 22 2212800, E-mail: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz,
Website: www.brela.go.tz

# Wanawake Masasi wahamasishwa kurasimisha biashara




*Msaidizi wa Usajili Bw. Suleiman Suleiman (kulia), akiwasilisha mada.*

**Na Roida Andusamile**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewataka wanawake wajasiriamali wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kusajili kampuni na majina ya biashara ili biashara zao zitambulike kisheria.

Rai hiyo imetolewa na Msaidizi wa Usaijili wa BRELA Bw. Suleiman Suleiman wakati akitoa elimu kwa wanawake wajasiriamali 110 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliyofanyika hivi karibuni wilayani humo.

Bw. Suleiman alisema pamoja na changamoto wanazokumbana nazo wajasiriamali wengi katika kutumia mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao, BRELA iko tayari wakati wote kutoa usaidizi. Hivyo, wanapokwama wasisite kuwasiliana na BRELA kupitia kituo cha miito ya simu ili kupatiwa usaidizi.

Bw. Suleiman alisema BRELA imekuwa ikitoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo wajasiriamali ili kuhakikisha kuwa wadau wote wananufaika kutokana na sajili pamoja na leseni zinazotolewa na BRELA.

"Kuna manufaa mengi ambayo mnaweze kupata kutokana na kurasimisha biashara zenu kwani mbali na kulindwa kisheria pia kuna fursa za kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha pamoja kupata zabuni mbalimbali serikalini", alifafanua Bw. Suleiman.

Kwa upande wake Msadizi wa Usajili wa BRELA Bw. Athuman Makuka aliwaelimisha wanawake hao umuhimu wa kuwa na alama za biashara katika bidhaa zao ili ziweze kutambulika.

Alisema watakaposajili alama za biashara itakuwa rahisi kwa bidhaa zao kujitofautisha na nyingine, hivyo kuwa na uhakika na soko la bidhaa zao. Usajili pia utamuwezesha mjasiriamali kupata haki ya kipekee ya alama ya biashara au huduma ambayo itasaidia kuzuia wengine kutumia alama yake sokoni ili kujipatia manufaa kinyume na sheria lakini pia itamuwezesha mjasiriamali kuhimili soko la ushindani kwa kuwa itakuwa ni rahisi wateja kutambua bidhaa yake sokoni.

Naye Afisa Leseni wa BRELA Bw. Jubilate Muro aliwasihi wajasiriamali kusajili viwanda vidogo BRELA kwani katika wilaya hiyo wengi wao wana viwanda vidogo vya kubangua korosho, kutengeneza sabuni na batiki ambavyo kisheria vinapaswa kusajiliwa.

Awali akifungua mafunzo hayo Mbunge wa Viti Maalum (UWT) mkoa wa Mtwara Mhe. Agnes Hokororo alishukuru jitihada zinazofanywa na BRELA kuwafikia wadau mahali walipo na kuwapatia elimu.

Mhe. Hokororo alisema kwa kuwa wanawake wengi wilayani humo wamejikita katika sekta isiyo rasmi ili waweze kujikomboa kiuchumi, mafunzo haya yamefika wakati muafaka kwani watanufaika na kuwa mabalozi wa kufikisha elimu ya BRELA kwa wengine.

Mhe. Hokororo alikiri kuwa wajasiriamali wengi wilayani humo hawajasajili majina ya biashara. Hivyo, elimu ya BRELA itawawezesha kufuata utaratibu wa kusajili majina ya biashara.

Wanawake wajasiriamali wa Halmashauri hiyo walipatiwa elimu kuhusu Usajili wa Majina ya Biashara na Kampuni, Alama za Biashara na Huduma na jinsi ya kupata leseni za biashara na viwanda.

Semina hiyo ya siku moja iliratibiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

# Wajasiriamali lindeni biashara kisheria - BRELA

**Na Theresa Chilambo**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewahimiza wajasiriamali mkoani Tanga kulinda biashara zao kisheria kwa kusajili Alama za Biashara na Huduma wanazotoa, ili waweze kutambulika katika masoko na kuzilinda kisheria.

Ushauri huo ulitolewa na Afisa Usajili wa BRELA, Bi. Julieth Kiwelu, kwenye mafunzo ya wajasiriamali yaliyofanyika sambamba na Maonesho ya Biashara, Utalii na Uwekezaji katika uwanja wa Mwahako, jijini Tanga.

Bi. Kiwelu alieleza kuwa mjasiriamali anaposajili Alama ya Biashara na Huduma inamsaidia bidhaa yake kutambulika katika masoko na inamlinda mjasiriamali kumiliki alama ya bidhaa kisheria, hivyo ni kosa kisheria kwa mfanyabiashara mwingine kutumia jina au alama inayofanana na bidhaa yake.

Aliwasisitizia wajasiriamali kusajili Alama za Biashara na Huduma ili bidhaa zao ziweze kutofautishwa na bidhaa nyingine zinazozalishwa, zenye ufanano na usajili huo utasaidia kwenye ushindani wa kimasoko.

Pia, katika mafunzo hayo aliwaeleza washiriki kuhusu umuhimu wa kusajili Majina ya Biashara ili kutambulika kisheria, hatua itakayowawezesha kupata huduma nyingine kutoka taasisi mbalimballi zikiwemo za fedha.



*Afisa Usajili wa BRELA, Bi. Julieth Kiwelu (kushoto) akitoa mafunzo kwa wajasiriamali jijini Tanga*

Katika mafunzo hayo wajasiriamali hao pia walipata elimu juu ya utaratibu wa kupata Hataza, Leseni za Biashara kundi "A" na Leseni ya Kiwanda na usajili wa Kiwanda Kidogo.

BRELA ilishiriki kwenye Maonesho ya Biashara, Utalii na Uwekezaji ikitoa huduma za sajili, utoaji wa leseni, elimu na ushauri kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kwa ujumla.



*Baadhi ya wajasiriamali wakifuatilia mafunzo wakati wa Maonesho ya Biashara Utalii na Uwekezaji ya Tanga*

# Wajasiriamali wanawake wapata elimu BRELA

**Na Lugano Mwakyombe**




*Afisa Sheria kutoka BRELA Bi. Neema Nyadzi akiwasilisha mada*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa Elimu kwa Umoja wa Wanawake Wajasiriamali (Tanzania Women Empowerment Network -TAWENI), juu ya Umuhimu wa Usajili wa Biashara na Leseni, katika ukumbi wa Saba Saba Jijini Dar es Salaam.

Akiwasilisha mada katika kuadhimisha mwaka mmoja wa Umoja wa Wajasiriamali Wanawake Tanzania - (TAWENI), Afisa Sheria kutoka BRELA Bi. Neema Nyadzi aliwahimiza wanawake wajasiriamali kusajili biashara zao. Bi, Nyadzi alisema;

"Nawashauri wanawake wenzangu, kusajili biashara zenu ili zitambulike kisheria. Kusajili jina la biashara, kunakupa fursa mbalimbali zikiwemo, kupata zabuni na tenda mbalimbali.

Pia alieleza kuhusu faida nyingine zinazotokana na usajili wa jina la biashara kuwa ni pamoja na kutambulika katika nyanja ya biashara.

Zaidi ya hapo Bi. Nyadzi alieleza nmna ya kujisajili kupitia Mfumo wa Mtandao wa BRELA ujulikanao kama ORS

Akipongeza jitihada zinazofanywa na Serikali kupitia (BRELA), mmoja wa wajasiriamali anayejishughulisha na usindikaji na uchakataji wa nafaka, kutoka Mbagala, Bi, Asia Mfaume aliishukuru BRELA kwa mchango wake mkubwa wa kutoa Elimu na kulinda Alama zao za Biashara kisheria kupitia usajili.

Mjasiliamali hiyo aliongeza kuwa, amechukulia hii kuwa fursa ya kuweka Usalama na uhakika katika bidhaa zake.

Semina hiyo ililenga kuwaunganisha na kuwapa fursa wanawake wajasiliamali kupata elimu kutoka katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii.



*Afisa Sheria wa BRELA Bi. Neema Nyadzi akimpatia maelekezo mmoja wa washiriki wa mkutano huo jinsi ya kuingia katika Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS)*

**"Nawashauri wanawake wenzangu, kusajili biashara zenu ili zitambulike kisheria. Kusajili jina la biashara, kunakupa fursa mbalimbali zikiwemo, kupata zabuni na tenda mbalimbali.**

# BRELA yasaidia watoto wenye uhitaji



*Watumishi wa BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na watoto wa kituo cha AL-Azam Orphanage Centre kilichopo Mbagala Zakhiem walipofika kituoni hapo kutoa misaada mbalimbali kwa watoto hao.*

**Na Christina Njovu**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa mahitaji katika kituo cha watoto wenye uhitaji cha AL-Azam Orphanage Center kilichopo Kata ya Mbagala Zakhiem Wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam. Baadhi ya mahitaji yaliyotolewa ni pamoja na mafuta ya kupikia, sabuni, sukari, unga wa sembe, mchele, maharage, nyama, madaftari, dawa ya meno, miswaki, pipi na kalamu.

Afisa Leseni Bw. Koyan Abubakar kutoka BRELA kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu aliwaeleza kuwa lengo kubwa ni kuwatia moyo watoto na uongozi wa kituo hicho kwa kazi kubwa wanayoifanya ili kuongeza juhudi ya kuwahudumia wahitaji ili kufikia ndoto zao. "BRELA ni taasisi inayosimamia usajili wa Biashara na Leseni, imefika katika kituo hiki kwa kuwa ni sehemu ya utaratibu wa taasisi kushirikiana na jamii sio tu kutoa huduma za sajili, lakini pia kutoa huduma za kijamii" alisema Koyan.

Naye Afisa Msajili Mwandamizi, Lugano Mwampeta aliwaeleza watoto wanaolelewa katika kituo hicho baada ya kueleza ndoto zao katika moja ya nyimbo walizoimba kuwa, njia kuu ya kuzifikia ndoto zao ni kwa kufuata mafundisho wanayofunzwa na walezi wao hapo kituoni.

"Njia kuu ya kufikia ndoto zenu ni kufuata mafundisho yanayotolewa na walezi wenu hapa kituoni; pili ili muweze kufikia ndoto hizo ni kufanya bidii katika masomo yenu shuleni", alisema Bw. Mwampeta.

Mkurugenzi wa kituo cha watoto wenye uhitaji na waishio katika mazingira hatarishi cha AL-ZAM Orphanage Center Bi. Zainab Said Buleta, aliishukuru BRELA kwa msaada huo ambao alisema

**"Njia kuu ya kufikia ndoto zenu ni kufuata mafundisho yanayotolewa na walezi wenu hapa kituoni; pili ili muweze kufikia ndoto hizo ni kufanya bidii katika masomo yenu shuleni", alisema Bw. Mwampeta.**

utawawezesha watoto hao kujikimu.

Bi. Zainab alieleza kuwa, kituo hicho kilianza kulea watoto 10, watano wakiwa ni wa kike na watano wakiume. Hivi sasa kituo kina jumla ya Watoto 60, Watoto 35 wasichana na wavulana 25 ambao wanaishi katika kituo hicho. Pia wapo baadhi ya watoto wanaoishi nyumbani kwao lakini wanahudumiwa kila kitu kutokea kituoni hapo.

# Fahamu umuhimu wa Kampuni kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa

- Ni wajibu kisheria
- Wahariri waelimishwa



*Baadhi ya wahariri wakifuatilia mada mbalimbali za kuhusu Miliki Manufaa.*

**Na Mwandishi Wetu**

Hivi karibuni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ilikutana na Wahariri wa Vyombo vya Habari mbalimbali, jijini Dar es salaam.

Lengo kuu lilikuwa ni kuwajengea Wahariri uelewa juu ya dhana ya Wamiliki Manufaa(Benefial Owners) na hatimaye kuhamasisha wamiliki wa kampuni kuwasilisha taarifa za Wamiiki Manufaa.

Sheria ya Kampuni inabainisha kuwa Mmiliki manufaa ni mnufaika wa mwisho wa Kampuni, ambaye wanamiliki au ana maamuzi katika Kampuni.Ikiwa kuna shaka, kampuni inapaswa kutafuta ushauri wa kisheria ili kuisaidia kubaini wamiliki wake wanaofaidi ni akina nani.

Akizungumza katika mafunzo hayo , Kaimu Mkurugenzi wa Makampuni na Majina ya Biashara Bw. Meinrad Rweyemamu, amesema kuwa lengo la kukutana na wahariri wa vyombo vya habari ni kuwajengea uelewa na kujadili majukumu ya BRELA pamoja na kuongeza ushirikiano katika utendaji.

Bw. Rweyemamu amesema kuwa vyombo vya habari ni muhimu katika kuelimisha umma kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA, hivyo dhana ya wamiliki Manufaa inapaswa kueleweka vyema kwa wadau kwani taarifa za Wamiliki Manufaa zinapaswa kuwasilishwa kwa mujibu sharia.

Bw. Rweyemamu amesema kuwa taarifa za Mmiliki Manufaa zinatakiwa ili pia kumfahamu mtoa maamuzi katika kampuni kwa lengo la kupunguza mianya ya utakatishaji fedha na kutambua vyanzo vya fedha vya wamiliki wa kampuni kwa usalama wa Taifa na uchumi kwa Ujumla.

“Kuna baadhi ya wamiliki wa kampuni wanaonekana katika mfumo ila katika uhalisia siyo wamiliki halali, hivyo ni

**"Kuna baadhi ya wamiliki wa kampuni wanaonekana katika mfumo ila katika uhalisia siyo wamiliki halali, hivyo ni vyema taarifa hizi zikawakilishwa kwa Msajili Ili Mmliki Manufaa atambulike, kwani kuna uwezekano mkubwa kuwa mtu anamiliki kampuni lakini hataki kujulikana, hivyo taarifa hizi zitasaidia kumjua Mmliki Manufaa ni nani katika kampuni," amefafanua Bw. Rweyemamu.**

vyema taarifa hizi zikawakilishwa kwa Msajili Ili Mmliki Manufaa atambulike, kwani kuna uwezekano mkubwa kuwa mtu anamiliki kampuni lakini hataki kujulikana, hivyo taarifa hizi zitasaidia kumjua Mmliki Manufaa ni nani katika kampuni," amefafanua Bw. Rweyemamu.

Amesema kuwa awali mfumo ulikuwa unapokea taarifa bila kujali mtaji unatoka wapi, hivyo suala hili likawa chanzo cha mianya ya rushwa na tishio la kiusalama, ndiyo maana sheria ya Makampuni ilifanyiwa marekebisho na kuweka kipengele kinachozilazimu kampuni kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa.

"Dhana hii ni nzuri na ni lazima ifahamike kwa wadau na wamiliki wa kampuni, kwani inatoa wigo kwa Serikali kufanya maamuzi sahihi kama kuzuia masuala ya utakatishaji fedha, rushwa, kupanga kodi, pamoja na kuzuia mianya ya ugaidi, Dunia nzima inaelekea huko, hatuna budi kuelekea huko," amesema Rweyemamu.

Amesema kuwa taarifa za Wamiliki Manufaa zinapaswa kuwasilishwa kwa wakati kwani muda wa uwasilishaji uliongezwa na Serikali Ili kufanikisha suala hilo. Aidha, amewaomba Wahariri wa Vyombo Mbalimbali vya Habari nchini walioshiriki katika mafunzo hayo kutoa mwanga kwa wadau wengine Ili dhana hiyo ieleweke vema kwa manufaa ya taifa la Tanzania

Naye Mkuu wa Sehemu ya Usajili wa Makampuni, Bw. Isidory Nkindi amesema BRELA imekuwa ikifanya maboresho mbalimbali ya kisheria na mifumo kutokana na kuthamini mchango wa makampuni kwenye kuchangia uchumi wa nchi, huku akikemea baadhi ya kampuni zinazokwepa kodi.

"Sheria ya kampuni sura ya 212 ilifanyiwa marekebisho kupitia sheria ya fedha 2020 kwa kuleta dhana ya umiliki manufaa wa kampuni, marekebisho yalienda sambamba na utungwaji kanuni za wamiliki manufaa mwaka 2021 za kusimamia utekelezaji wa uwasilishaji wa taarifa Mmiiki Manufaa wa kampuni," amesema Nkindi.

Wakati huo huo, Msajili Msaidizi wa BRELA Bi. Leticia Zavu amewataka wamiliki Kampuni kuhuisha taarifa za kampuni zao kwani muda wa kwanza uliotolewa umepita.

Bi. Zavu amesema zoezi la kuhuisha taarifa za makampuni lilianza rasmi mwaka 2018 lakini bado muitikio ni mdogo hivyo ni vema wahusika wakatekeleza takwa hilo la muhimu kisheria.

"Brela inatoa wito kwa wamiliki Kampuni kuhuisha taarifa zao ili tuwe na taarifa sahihi kuhusu kampuni yako kwasababu kuna mambo muhimu kama vile kampuni kuwa na mikopo, kubadili wamiliki manufaa , ongezeko la mtaji na wanahisa,hivyo ni muhimu sana kuhuisha taarifa za kampuni tunazomiliki,"amesisitiza Bi. Zavu

Kuhusu ukomo wa muda wa Wamiliki wa Makampuni kuwasilisha taarifa zao, Bi. Zavu amesema kwamba kwa sasa hakuna muda maalumu lakini ni vyema wakaharakisha ili BRELA itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa manufaa ya wamiliki Manufaa na kampuni zao.



*Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Bw. Deodatus Balile (aliyeketi katikati), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wahariri wa vyombo vya habari, baada ya ufunguzi wa mafunzo kuhusu Wamiliki Manufaa yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam. Aliyeketi kulia ni Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA Bw. Andrew Mkapa na kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara wa BRELA, Bw. Meinrad Rweyemamu.*


BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
BRELA HOUSE
*152*00#
Chagua 9
Kisha 2
Pakua
eMrejesho
Mobile App
Ingia katika
Google play
Tafuta eMrejesho
Jengo la BRELA, Kitalu Na 20, Nyumba Na 23,
Barabara ya Sokoine / Mtaa wa Shaaban Robert , S.L.P. 9393,
11101, Dar es Salaam. Simu: +255-22 2212800,
barua pepe: maoni@brela.go.tz, malalamiko@brela.go.tz
usajili@brela.go.tz
Tovuti: www.brela.go.tz
BRELA tanzania
Brela _tanzania
brela _tanzania
brela _tanzania